**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA TISA

**15 NOVEMBA, 2019**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA TISA – TAREHE 15 NOVEMBA, 2019

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MAAZIMIO:**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Maelezo ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kinga na Maslahi ya Kidiplomasia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kinga na Maslahi ya Kidiplomasia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kinga na Maslahi ya Kidiplomasia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Maelezo ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Afrika Mashariki ya Mitandao ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Afrika Mashariki ya Mitandao ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Afrika Mashariki ya Mitandao ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

## III. MASWALI:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**110. MHESHIMIWA PROSPER JOSEPH MBENA (MOROGORO KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Shule ya Sekondari ya Milengwelengwe katika Kata ya Mngazi ilijengwa mwaka 1997 na ina Wanafunzi 412 wa bweni. Nyakati za mvua Shule hiyo inakumbwa na mafuriko kila mara na kufanya eneo la Shule kujaa maji kutokana na ukosefu wa mitaro mikubwa ya kuondoa maji hayo hivyo Walimu na Wanafunzi kuathirika na hali hiyo na pia majengo ya Shule huendelea kuharibika:-

Je, Serikali iko tayari kutenga fedha za kutosha kutengeneza miundombinu itakayomaliza tatizo hilo.

**111. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kumekuwa na mafuriko yanayoleta madhara mpaka vifo barabara ya Dodoma katika Jiji la Arusha hasa katika Kata ya Sombetini eneo la Majengo ya Chini pamoja na eneo la Esso Road:-

Je, ni lini Serikali kupitia mamlaka zake itaokoa maisha ya Wakazi wa maeneo hayo.

**112. MHESHIMIWA JOHN JOHN MNYIKA (KIBAMBA)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Matengenezo ya barabara katika Halmashauri mbalimbali yamekuwa yakisuasua tangu TARURA ilipokabidhiwa kazi hiyo:-

(a) Je, ni hatua zipi Serikali inazichukua kuhakikisha TARURA inapata fedha za kutosha ili kuongeza ufanisi wa matengenezo ya barabara;

(b) Je, ni barabara zipi zimekabidhiwa kwa TARURA lakini hazijazifanyiwa matengenezo ya kutosha katika Jimbo la Kibamba na ni lini zitatengenezwa;

(c) Je, ni lini barabara ya kwa Msuguri – Temboni – Msingwa itajengwa kwa kiwango cha lami.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

**113. MHESHIMIWA SILAFU JUMBE MAUFI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Jitihada

za Serikali za kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya kwa Wananchi wake zinaonekana kwani kila mwaka huongeza bajeti ya Wizara ya Afya kwa ajili ya dawa, vifaa tiba, vitendea kazi na majengo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuajiri Watumishi watoa huduma wakati majengo ya kutolea huduma yapo na yanaongezeka.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**114. MHESHIMIWA SUSAN ANSELM LYIMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Mfumo wetu wa elimu umekuwa ukilalamikiwa na kukosolewa sana:-

Je, Serikali imefanya utafiti wowote kuona kama lawama hizi zina mashiko au la.

**WIZARA YA NISHATI:**

**115. MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MASWA MAGHARIBI)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Kumekuwa na tatizo la transfoma zinazowekwa na Wakandarasi wa umeme wa REA kulipuka na kuharibika haraka sana:-

Je, Serikali inachukua hatua gani juu ya kuondoa tatizo hili.

## WIZARA YA MADINI:

**116. MHESHIMIWA MAGDALENA HAMIS SAKAYA (KALIUA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:- Tafiti mbalimbali zilizofanywa ndani na nje ya nchi zimethibitisha kuwepo kwa madhara makubwa ya kiafya, kimazingira n.k. katika matumizi ya madini ya zebaki kuchenjulia dhahabu:-

Je, Serikali inasemaje juu ya kuendelea kutumika kwa madini hayo hapa nchini.

## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

**117. MHESHIMIWA EDWARD FRANZ MWALONGO (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Itoni – Lusitu katika Jimbo la Njombe Mjini.

**118. MHESHIMIWA MAHMOUD HASSAN MGIMWA (MUFINDI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya

Kinyanembo – Isalavam – Igombavam – Sedani – Madibira hadi Rajon ni muhimu kwa uchumi wa Wananchi wanaotoka katika maeneo ya Mbozi na Iringa na imekuwepo katika Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2005, 2010 na 2015 lakini mpaka sasa hata kilomita moja ya lami haijajengwa:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi hiyo ya uchaguzi.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE, NA WATOTO:**

**119. MHESHIMIWA FAIDA MOHAMMED BAKAR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Wanawake wengi walioachika pamoja na Wajane na Watoto wao hutelekezwa na kukosa matumizi kwa Baba zao na kusababisha Watoto hao kukosa huduma muhimu kutoka kwa Baba zao na kupelekea Wazazi hao wa kike kuteseka na Watoto peke yao:-

Je, Serikali inatoa tamko na hatua gani kwa Wababa wanaotelekeza Watoto.

## WIZARA YA MAJI:

**120. MHESHIMIWA EMMANUEL PAPIAN JOHN (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Bwawa la Dongo litaanza kuchimbwa ili kusaidia Wananchi wa maeneo hayo kupunguza adha ya ukosefu wa maji.

**121. MHESHIMIWA ENG. EDWIN AMANDUS NGONYANI (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- Wilaya ya Namtumbo inasumbuliwa na ukosefu wa maji kwa muda mrefu takribani miaka 13 sasa katika maeneo mengi kama vile Vijiji vya Mgombasi, Ligera, Libango, Matepwende ya Msisima na Vijiji vingine vingi:-

Je, Serikali inasaidiaje Wananchi wa Wilaya ya Namtumbo kuondokana na tatizo sugu la maji.

**122. MHESHIMIWA IGNAS ALOYCE MALOCHA (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itajenga mradi wa maji wa Kijiji cha Mkunda utakaohudumia Vijiji vya

Kaengesa A, Kaengesa B, Itela na Mkunda yenyewe.

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

**123. MHESHIMIWA HAWA ABDULRAHMAN GHASIA (MTWARA VIJIJINI)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-
Je, ni kwa nini fursa ya kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa itolewe kwa Vijana wachache na sio wahitimu wote wa Kidato cha Sita.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**124. MHESHIMIWA MARIA NDILLA KANGOYE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Asilimia kubwa ya Wafungwa Magerezani ni Vijana ambao mara nyingi wamekuwa wakirudi kwenye uhalifu baada ya vifungo vyao kwa kukosa shughuli za kufanya:-

Je, kwa nini Serikali isianzishe michezo Magerezani ili kujenga vipaji vitakavyoweza kuwasaidia hapo baadae.

## IV. HOJA YA BUNGE:

**AZIMIO:**

**MWAKILISHI WA TUME YA UTUMISHI WA BUNGE:**

Azimio la Bunge la Kumpongeza Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Job Y. Ndugai, kwa uamuzi wake wa kulifanya Bunge kutekeleza kwa vitendo dhana ya Bunge Mtandao *(e-Parliament).*

## V. HOJA ZA SERIKALI:

**MAAZIMIO:**

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kinga na Maslahi ya Kidiplomasia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Azimio la Kuridhia Itifaki ya Afrika Mashariki ya Mitandao ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

**SAA 10:00 ALASIRI**

**AZIMIO LA BUNGE:**

Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Utendaji uliotukuka kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wake.

**VI. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:**

**VII. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:**

**WAZIRI MKUU.**

**VIII. WIMBO WA TAIFA.**

**DODOMA**
**15 NOVEMBA, 2019**

**S. KAGAIGAI**
**KATIBU WA BUNGE**